



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA MAJI

CHUO CHA MAJI



UTARATIBU WA MAHAFALI KWA WAHITIMU-2026

Wahitimu wote mnataarifiwa kuwa Mahafali ya **50** ya **Chuo cha Maji** yatafanyika tarehe **02 Disemba, 2026** katika **Ukumbi wa Mlimani City** kuanzia **saa 3:00** asubuhi. Tafadhali zingatieni maelekezo yafuatayo;

- i. Wahitimu wote mnatakiwa kuhakiki Majina yenu kwenye mfumo wa **SIMS** kuanzia leo tarehe **12/10/2026** hadi **23/10/2026**, majina hayo yasomeke kama yalivyo katika cheti cha kidato cha nne. Taarifa zote muhimu zijazwe kwa usahihi ikiwemo mwaka wa kuzaliwa, sanduku la posta, mwaka wa kuanza masomo na picha ya **passport size yenye kivuli cha blue**. Marekebisho yote ya majina yatumwe kwenye barua pepe: dass@waterinstitute.ac.tz.
- ii. Kadhalika, kila mhitimu anatakiwa kuthibitisha ushiriki wake katika mahafali kwa kulipa kiasi cha **Tsh. 45,000/=** kupitia **Control Number** atakayoitengeneza katika akaunti ya SIMS. Malipo hayo yanahusisha ukodishaji wa Joho la Mahafali na yatumika kama uthibitisho rasmi wa ushiriki wa mhitimu katika mahafali. Mwisho wa kufanya uthibitisho ni tarehe **20/11/2026**.
- iii. **Fomu ya Kuazima Joho:** Wahitimu wote wanatakiwa kujaza fomu ya kuazima joho inayopatikana katika tovuti ya Chuo. Hakikisha umeambatanisha risiti ya malipo iliyotolewa na **Ofisi ya Uhasibu** kabla ya kuwasilisha fomu siku ya kuchukua joho.

- iv. **Ugawaji wa Joho:** Majoho yatagawiwa tarehe **30 Novemba** hadi **01 Disemba, 2026** kuanzia saa **4:00** hadi saa **10:00** kamili jioni. Mwisho wa kurejesha majoho ni tarehe **10 Disemba, 2026** saa **10:00** jioni.
- v. **Wazazi/Walezi:** Kila mhitimu anaruhusiwa kuingia ukumbini na mzazi au mlezi mmoja tu.
- vi. **Muda wa Kuingia:** Wazazi na wahitimu wanatakiwa kufika mapema kwani milango ya kuingia ukumbini itafunguliwa saa **2:00 asubuhi** na kufungwa saa **2:30 asubuhi**. Tafadhali zingatia muda ili kuepuka usumbufu.
- vii. **Zingatia Utulivu:** Mara mahafali yatakapoanza hakutakuwa na ruhusa ya kutoka nje ya ukumbi. Mtu yeyote atakayetoka nje kwa dharula yeyote hataruhusiwa kurudi ukumbini.
- viii. **Baada ya wimbo wa Taifa** hakuna mhitimu atakayeruhusiwa kuingia ndani ya ukumbi.
- ix. **Rehearsal:** Kutakuwa na mazoezi ya mahafali (rehearsal) tarehe **01 Disemba, 2026**, saa **8:00 mchana** katika **Ukumbi wa Mlimani City**. Wahitimu wote wanatakiwa kuhudhuria bila kukosa.

Tafadhali zingatia maelekezo haya ili kufanya siku hii kuwa ya mafanikio na ya kukumbukwa kwa kila mmoja. Karibuni sana na tunatoa pongezi nyingi kwa hatua mliyofikia!

Imetolewa na:
Kitengo cha Mawasiliano na Masoko
12/10/2026